

Waziri aipa jukumu TAFIRI kufanikisha uvuvi wenyе tija

NA RUKIAH MOHAMED (TUDARCO)

TAASISI ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), imetakiwa kufanya kazi zenye tija kwa jamii na kutoa ushauri wa kisayansi kuhusu ukuaji wa sekta hiyo na kusaidia Watanzania.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashiriba Ndaki, wakati wa ziara yake ya kikazi aliyopifanya katika Makao makuu ya taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam.

Alibainisha kwamba TAFIRI inategemewa katika kufanya utafiti wa uvuvi kwa manufaaa ya sasa na yajayo ili kuwafanya wavuvi kuwa na kipato endelevu kupitia

uvuvi wa kitaalamu.

Ndaki alipongeza Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFISH), ambao umewezesha kujengwa kwa jengo la maabara ya TAFIRI litakaloongeza wigo katika kufanya utafiti wa uvuvi nchini.

Alifafanua mradi huo umekuwa ukifanya kazi muhimu, ikiwemo kuhakikisha usimamizi wa fedha zilizotolewa na Benki ya Dunia kufanikisha mradi huo.

Hata hivyo, Waziri Ndaki aliahidi katika mwaka wa fedha ujao, atahakikisha vifaa vya maabara kwa ajili ya kufanikishia shughuli za utafiti vinapatikana.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TAFIRI, Dk. Ishmael Kimirei, alisema baada ya jengo hilo kukamilika wanakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo uhaba wa vifaa ambavyo thamani yake ni sh. bilioni 1.5.

Naye, Mratibu wa mradi wa SWIOFISH, Nichrous Mlalila, alisema mradi huo wa miaka sita nchini, unaotarajia kufikia tamati Septemba mwakani, umefadhiliwa na Benki ya Dunia, ukilenga kusimarnia masuala ya uvuvi kuanzia ngazi ya utawala hadi kwa wavuvi na kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika kuhakikisha unaboresha mnyororo wa thamani wa mazao ya uvuvi.

By Felister Peter, Dodoma

PRIME Minister Kassim Majaliwa told the National Assembly here yesterday that the newly introduced livestock identification and traceability system which includes tagging of animals with ear tags will reduce incidences of livestock theft.

He said apart from labeling animals with ear tags, the government has also tightened measures for transportation of livestock from one village to the other. He said animal transporters are required to acquire permits from local government authorities.

The ear tagging procedure has been identified as the key identification device which enables farmers as well as authorities to identify the animals' origin and

Ear tags will reduce prevalence of livestock thefts, premier says

the owner," he said adding the ear tags are an alternative to the previous animal identification and traceability system whereas animals were labeled through heat branding.

He said the government resolved to shift from the traditional branding method for cows, goats and sheep to ensure quality of the produced animal skins. He said previously, there were complaints from leather factories that some locally produced animal skins were at low quality due to the use of traditional branding methods.

Majaliwa noted that during his recent meeting with livestock stakeholders in Dar es Salaam, they agreed that placing of ear tags should not include ear mutilation. He said to reduce cost of the ear tags, livestock keepers will only pay once for the tracing devices and that if misplaced farmers will only need to present documents indicating they had paid for the devices previously.

He was responding to a query raised by Nkasi North Member of Parliament (CHADEMA) during the impromptu questions and

answers session. The legislator was concerned that livestock keepers were supposed to pay at least 1,700/- for each of the ear tags, and that if lost they would be forced to repay the money. Kenan requested the government to reduce the price of ear tags to allow livestock keepers to protect their animals.

The government has in the 2021/2022 financial year introduced the new ear tag identification and traceability system which has now started to be applied in some regions including Rukwa. *

Govt to form livestock authority to cater for pasture, markets

By DAILY NEWS Reporter

THE government will establish a livestock authority that will ensure pasture is readily available to livestock and keepers get markets for animals and their products.

Minister for Livestock and Fisheries Mashimba Ndaki told a meeting of stakeholders here that the government remains keen on improving livestock keeping environment so that the sector can make bigger contribution to national development.

"The government will form an authority that will essentially oversee availability of pasture and look livestock products markets," he told delegates to a livestock stakeholders' meeting that ended here yesterday.

He added that the authority: "will work to improve this sector, reduce conflicts and stop livestock keepers from roaming around the country."

In the past three decades, Tanzania has witnessed widespread and sometimes bloody clashes between farmers and wandering herders looking for grazing land and water for animals. Animals have intermittently on and off encroached on farms, eaten crops and trampled on water sources.

Mr Ndaki told the delegates that the planned authority will deal with those and other problems and that he was using the

forum to assure livestock keepers that the government has their interests at heart.

"I am here to encourage you and assure you that the government is there and will continue to improve conditions for keeping livestock in recognition of its importance in advancing our economy and in creating jobs for the youth," he said.

The Tanzania Agricultural Development Bank (TADB) Acting Director for Planning, Research and Policy, Mr Mzee Kilele, who stood for the Bank's Managing Director, Mr Frank Nyabundege, assured delegates of the bank's support.

He explained that meetings of that nature give the TADB the information it needs to reach and serve many livestock keepers.

"I am using this opportunity to assure delegates that our bank will increase pace in providing loans and adding value to livestock products so that the sector becomes strong, it benefits the herders themselves and promotes national economy," he said.

Until August this year, Mr Kilele said, the TADB had given the sector direct loans amounting to 23.8bn/-, enabling 128 farmers in five AMCOs to secure high breed cows. The bank has also disbursed 11.8bn/-, helping recipients to build four dairy industries that buy milk from over 6,000 farmers.

Govt to form livestock authority to cater for pasture and markets

By **Guardian Reporter**

THE government will establish a livestock authority that will ensure pasture is readily available to livestock and keepers get markets for animals and their products.

Minister for Livestock and Fisheries Mashimba Ndaki told a meeting of stakeholders here that the government remains keen on improving livestock keeping environment so that the sector can make bigger contribution to national development.

"The government will form an authority that will essentially oversee availability of pasture and look for markets for livestock products", he told delegates to a livestock stakeholders' meeting that ended here yesterday and added that the authority "will work to improve this sector, reduce conflicts and stop livestock keepers from roaming the country."

In the past three decades, Tanzania has witness widespread clashes between farmers and wandering herders looking for grazing land and water for animals. Animals have intermittently on and off encroached on farms, eaten crops and trampled on water sources.

Ndaki told the delegates that the planned authority will deal with those and other problems and that he was using the forum to assure livestock keepers that the government has their interests at heart. "I am here to encourage you and assure you that the government is there and will continue to improve conditions for keeping livestock in recognition of its importance in advancing the our economy and in creating jobs for the youth," he said.

The TADB Acting Director for Planning, Research and Policy, Mzee Kilele who stood for the Bank's Managing Director, Frank Nyabundenge, assured delegates of the bank's support, explaining that meetings of that nature give the Tanzania Agricultural Development Bank (TADB) the information it needs to reach and serve many livestock keepers.

"I am using this opportunity to assure delegates that our bank will increase pace in providing loans and adding value to livestock products so that the sector becomes strong, it benefits the herders themselves and promotes national economy," he said.

Until August this year, Kilele said, TADB has given the sector direct loans amounting to 23.8 billion, enabling 128 farmers in five AMCOs to secure high breed cows. The bank has also disbursed 11.8 billion, helping recipients to build four dairy industries that buy milk from over 6,000 farmers.

The chairman of Karagwe District Livestock Keepers Association Jackson Kamkoto said keepers lack requisite education on their trade, there a big shortage of extension officers and acute shortage of pasture and water for animals. He called on the government to form as institution that will coordinate issues relating to the livestock sector so that it becomes efficient and beneficial to the nation.

When opening the meeting, Premier Kassim Majaliwa called on the ministry of livestock and fisheries to participate fully in resolving conflicts between herders and other users of land.

“

I am using this opportunity to assure delegates that our bank will increase pace in providing loans and adding value to livestock products so that the sector becomes strong, it benefits the herders themselves and promotes national economy

Wavuvi wavua risasi 1,400 za SMG ziwani

Na Thobias Mwanakatwe

WAVUVI katika mwambao wa Ziwa Tanganyika wilayani Nkasi mkoani Rukwa, wamevua viboksi viwili ndani yake vikiwa na risasi 1,489 zinazotumiwa na bunduki aina ya SMG na nyingine za kivita.

Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Peter Lijualikali, akizungumza na gazeti hili jana kwa simu, alisema wavuvi hao kabla ya viboksi hivyo havijafunguliwa walidhani ndani yake kuna dhahabu.

"Jana (juzi) nilipokea simu asubuhi saa 2:00 kutoka kwa Mzee Jabile kwamba kuna wavuvi ambao amekuwa akishirikiana nao katika utafiti wa madini mwambao mwa Ziwa Tanganyika upande wa kijiji cha Kolongwe, ambao wamepata viboksi viwili na walipofungua kimojawapo wakakuta ni risasi, hivyo hawakuendelea kufungua cha pili," alisema.

Lijualikali alisema baada ya kupewa taarifa hiyo, yeye na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya walikwenda katika kijiji cha Kolongwe, na walipofika nyumbani kwa Mzee Jabile aliwakabidhi kiboksi kimoja alichokuwa nacho.

Alisema baada ya kukifungua walikuta kuna risasi 739, lakini kiboksi kingine kili-

chokuwa kimechukuliwa na mvuvi mwinge-
ine ambaye alipotakiwa kukileta ili kifun-
guliwa alikataa akitaka kwanza apewe fedha
kwani aliamini kuwa ndani yake kulikuwa
na mali (dhahabu).

"Mzee Jabile alitafuta fedha kiasi alichoku-
wa anakihitaji mvuvi huyo ambapo alimtu-
ma kijana wake ili akakikomboe kiboksi na
baada ya kupewa fedha alikitoa," alisema.

Lijualikali alisema kiboksi cha pili baada
ya kukifungua kilikutwa na risasi nyingine
750 na hivyo kufanya idadi ya risasi kuwa
1,489 zilizopatikana ndani ya viboksi hivyo.

Alisema baadaye yeye na kamati yake
walikwenda hadi mwambao wa Ziwa Tang-
anyika eneo vilipopatikana viboksi hivyo ku-
fanya uchunguzi zaidi, lakini hakubahatika
kupata viboksi vingine zaidi.

"Nimeviachia vyombo vyaya ulinzi na us-
alamu viendelee kuchunguza suala hili, na
kama kuna kosa lolote la kijinai vichukue
hatua kali kwa wahusika," alisema.

Kufuatia tukio hilo, Lijualikali ametoa
wito kwa wananchi wa Wilaya ya Nkasi
waliopo mwambao mwa Ziwa Tanganyika
wakiona kitu chochote ambacho sio cha
kawaida wasikimbilie kukifungua, badala
yake watoe taarifa kwa mamlaka ili wafanye
uchunguzi ni kitu gani.

DC Iringa achoma moto nyavu za uvuvi haramu

**Iringa
NA CATHERINE MBIGILII**

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Hassan Moyo, amechoma nyavu haramu 80 za kuvulia samaki katika Bwawa la Mtera zenyet thamani ya sh. 13,814,000 ambazo zilikamatwa katika kipindi cha Julai 2021 hadi Septemba mwaka huu.

Akitekeleza tukio hilo jana, mkuu huyo alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya wavuvi kuvua samaki kwa kutumia njia haramu ambazo zimekuwa zikileta madhara katika kuzaliana na kukua kwa samaki katika bwawa hilo.

Moyo alisema sio mara ya kwanza kuchoma nyavu haramu kwenye bwawa hilo, kwani katika kipindi cha Julai 2020 hadi Agosti 2021, uongozi wa Halmashauri wa Wilaya ya Iringa ulikamata nyavu haramu 11,538 zenyet thamani ya sh. 152,100,000.

"Kipindi hicho chote tumekuwa tukikamata nyavu aina ya timba, kokoro, gonga, kimila na nyavu chini ya nchi tatu ambazo mara nyingi ndio zimekuwa zikitumiwa na wavuvi haramu katika Bwawa la Mtera na kusababisa uchumi wa wananchi kuyumba kwa kiasi kikubwa...kama Serikali hatuwezi tukavumilia vitendo hivi," alisema mkuu huyo wa wilaya.

Alisema serikari imekuwa ikitoa elimu ya usimamizi shirikishi wa kulinda rasilimali za uvuvi na kudhibiti uvuvi haramu mara kwa mara kwa wavuvi ambapo zaidi ya wavuvi 249 na vikundi vitano vya BMU, wavuvi 103 wamefanikiwa kupata elimu ya udhibiti wa usafirishaji wa samaki wachanga kwa mujibu wa sheria.

Moyo alisema katika kuimarisha udhibiti wa wavuvi haramu na ulinzi wa rasimali za uvuvi katika Bwawa la Mtera kwa sasa limekuwa shirikishi na jamii kwa kuunda kikosi kazi cha kudhibiti uvuvi haramu kwa kuwa jamii hiyo inawajua wavuvi haramu na ni kazi rahisi kuwadhibiti chini ya uongozi wa kata.

"Lengo la kuunda kikosi kazi hicho ni kulinda samaki waliopo katika Bwawa la Mtera ambao ndio wamekuwa tegemeo kwa uchumi wa wananchi wa Kata ya Migoli na maeneo ya jirani hivyo bila mikakati maalumu samaki hawa watapotea katika bwawa hili," alisema.

Naye Diwani wa Kata ya Migoli, Benito Kuyugwa, alisema uvuvi haramu kumesababisha kushuka kwa uchumi wa wananchi wa kata hiyo na baadhi kuyakimbia makazi yao.

Kuyugwa alisema Migoli ya sasa sio ya miaka iliyopita kutokana na wananchi wake kukosa fedha na baadhi ya wavuvi kuvua samaki kwa njia haramu ambazo zimesababisha kupungua kuzalianakwa samaki katika Bwawa la Mtera na kushusha uchumi wa wananchi ambao wamekuwa wanategemea uvuvi kuendesha maisha yao.



Wazíri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (wapili kushoto), akisikiliza kwa makini maoni na michango mbalimbali iliyotolewa na wadau wa sekta hiyo jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni ni Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Ma Tumaini Magesa (wapili kulia) na (kulia) ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera. **PICHA MPIGAPICHA WETU**

Serikali kuanzisha mamlaka ya malisho ya mifugo

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ametangaza kwamba serikali itaunda mamlaka itakayoratibu na kusimamia malisho ya mifugo na kuyatafutia masoko mazao yanayotokana na sekta ya mifugo.

Amewaambia mukutano wa wadau wa mifugo uliomali-

izika jana kwamba serikali inajali maslahi ya wafugaji na kwamba itatekeleza mawazo ya wadau wa sekta ya mifugo katika kuboresha sekta hiyo na kutengeneza mazingira bora ya ufugaji ili sekta hiyo iendelee kutoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya taifa.

Waziri Ndaki alisema serikali inafikiria kuanzisha mamlaka itakayosimamia malisho na masoko ya mifugo

na mazao yake na kubainisha kuwa mamlaka hiyo itafanya bidii kuinua sekta hiyo pamoja kupunguza migogoro na kuhamahama kwa wafugaji.

"Serikali itaunda mamlaka hii na moja ya jukumu lake kubwa ni kuangazia malisho na kutafuta masoko ya mazao ya sekta hii ya mifugo," alieleza.

Kaimu Mkurugenzi wa Mipango na Utafiti wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo

Tanzania(TADB), Mzee Kilele, ambaye alimwakilisha Mku-rugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege kuwa amewahakikishia wadau wa sekta ya ufugaji ushirikianao kutoka TADB.

Alisema kwamba mikutano yenye malengo mazuri kama huo, inaipa benki yao fursa ya kujua, kutambua na kuona jinsi gani inaweza kuwafikia wafugaji wengi zaidi ili waweze kunufaika na fursa zitolewazo na benki hiyo.

Alieleza kuwa hadi Agosti mwaka huu, benki hiyo imetoa mikopo ya moja kwa moja kwenye sekta ya mifugo yenye thamani ya Sh bilioni 23.8 na fedha hiyo imewezesha AMCOS 5 kupata ng'ombe wa kisasa na kunufaisha wafugaji 128.

Aidha Kilele alisema kwa kuwa benki imetoa mikopo yenye thamani ya Sh bilioni 11.8 na fedha hiyo imeweze-sha ujenzi wa viwanda vinne vya maziwa.

"Kwa kutambua umuhimu wa sekta hii na uhusiano mkubwa baina ya sekta ya mifugo na maziwa tuliona ni vyema tutoe mikopo ambayo iliwezesha ujenzi wa viwanda vinne vya maziwa na wafugaji zaidi ya 6,000 itauza maziwa yao kwenye viwanda hivyo," alisema.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wafugaji Wilaya ya Karagwe, Jackson Kamkoto, alisema ukosefu wa elimu kwa wafugaji, uhaba wa maofisa ugani, uhaba wa malisho na maji zimekuwa changamoto kubwa zinazowakabili wafugaji nchini na kupende-keza serikali kuunda chombo maalumu kitakachoratibu masuala hayo ili kuongeza tija kwenye sekta ya ufugaji.

Akifungua mukutano huo Waziri Mkuu, Kassim Majali-wa aliitaka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kushiriki kikamilifu katika kutatua migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU
DAR ES SALAAM

SHAURI LA MADAI NO 79 YA 2021

THE BOARD OF TRUSTEES OF NATIONAL SEAL MDAI

SECURITY FUND

DHIDI YA

ULIDAKER CONSULTANCY AND BUSINESS INVESTMENT LTD.

KWA: THE MANAGING DIRECTOR

ULIDAKER CONSULTANCY AND BUSINESS INVESTMENT

P.O. Box 61614

DAR-E SALAAM

KUTWA SHAURINI

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya Mdai yameelezwa katika neka ya madai ambazo zinaweza kusatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo Unahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii bila au kwa Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusuwa, siku ya tarehe 13/19/2021 Saa 7.00 Mchana. Kwa mujibu wa madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutajwa shauri hilo ni lazima mlele hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

ANGALIA:

Kama hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea Kuitwa Shaurini, itawezeku kusikiliza bila wewe kuwepo.

Hati hi imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe Mwezi wa 2021.

HAKIMU MKAZI MKUU
KISUTU - DAR ES SALAAM

HAKIMU MKAZI MKUU
KISUTU - DAR ES SALAAM

SC003468